## Maswali na Majibu

1. Ni taifa gani lilitoka kwa uzao wa Ibrahimu?
   *Ni taifa la Israeli lililoitwa Wayahudi baadaye.*
2. Mungu aliahidi Wayahudi nchi gani? Mji mkuu ulikuwa gani?
   *Nchi ya Israeli. Mji mkuu ulikuwa Yerusalemu.*
3. Wayahudi walifanya nini Mungu alipotuma Mwanawe kuwa mwakozi na mfalme?
   *Walimkataa na kumsulibisha.*
4. Wayahudi waliadhibiwa namna gani mwaka 70 baada ya Kristo?
   *Yerusalemu iliharibiwa na Warumi halafu Wayahudi wakafukuzwa kutoka kwa nchi yao na kutawanyika kwa mataifa mengine ulimwenguni.*
5. Wayahudi walikaa kwa hizo nchi waliotawanywa kwa muda gani?
   *Kwa karibu miaka 2,000.*
6. Kwa vita vya 2 vya ulimwengu, nini mbaya sana ilifanyika kwa Wayahudi?
   *Hitla aliuuwa Wayahudi zaidi ya milioni 6.*
7. Nini ilifanyika tarehe 14:05:1948?
   *Taifa la Israeli lilisimamishwa na Wayahudi wakaanza kurudi kwa nchi yao.*
8. Nini itafanyika kwa Wayahudi kabla ya Yesu kukuja?
   *Mataifa mengi yatakuja kupigani na Waisraeli. Lakini Yesu atawaakoa.*
9. Wakati huu Wayahudi wanaamini kwa Yesu? Yesu atawaonyesha nini?
   *Hapana. Hawaamini kwa Yesu. Atawaonyesha alama za majeraha.*
10. Nani atakuwa mfalme wa Wayahudi? Nani atatawala makabila 12?
    *Yesu atakuwa mfalme wa Wayahudi. Wanafunzi 12 watatawala hizo makabila.*

## Mistari ya kukariri

Kumbukumbu 7:6 Yeremia 31:10 Zekaria 12:10

## Mazungumzo

Zungumza juu ya ahadi zenye Mungu alifanya na Ibrahimu na Daudi. Zungumza vile Mungu amekuwa akifanya kusudi zake ili atimize hizi ahadi.

## Kuandika

Andika juu ya kilichofanyika mwaka wa 70 baada ya Kristo tena kilichofanyika mwaka 1948.

# Masomo ya watoto wakubwa wa CBM

## Somo la 49 Kusudi ya Mungu kwa Waisraeli

**SOMA Kumbukumbu 7:6 – 10; 28:64 – 67; Yeremia 31:8 – 10; Ezekieli 37:21; Zekaria 12:9 – 10;**

**SOMO**

Kusudi ya Mungu ni kujaza dunia yote na watu wanaojua utukufu wake na waonyeshe mwenendo Wake katika maisha yao. Mungu amekuwa akionyesha kusudi yake tangu mwanzo.

Mungu alimchagua Ibrahimu, mtu wa imani kuu. Mungu aliahidi Ibrahimu kwamba uzao wake utakuwa taifa kubwa. Uzao wa Ibrahimu ulikuwa taifa la Israeli na walikuwa wateule wa Mungu. Mungu alichagua nchi ya Israeli kuwa nchi yenye Ufalme Wake utasimamishwa.

Wakati wa Musa, Mungu alipea taifa la Israeli amri 10. Mungu alifanya agano (mapatano) ya kipekee nao. Mungu aliahidi kwamba Waisraeli watakuwa watu Wake wa kipekee Naye atakuwa Mungu wao. Atawabariki na kuwalinda kwa hiyo nchi aliyowaahidi. Watu waliahidi kumpenda Mungu na kutii amri Zake. Lakini aliambia Waisraeli kwamba wakikataa kumtii na waabudu miungu mingine, atawafukuza watoke kwa hiyo nchi.

Wakati wa Daudi, mfalme bora, Mungu alichagua Yerusalemu kuwa mji mkuu wa Israeli. Mungu aliahidi Daudi kwamba, mmoja wa wazao wake atatawala kwa kiti chake cha enzi milele.

Baada ya muda mrefu, watu wa Israeli walikuwa waovu sana. Walikataa kutii amri za Mungu na wakaanza kuabudu sanamu. Mungu alituma mataifa za nguvu kama Ashuru na Babeli kuwatoa kwa nchi yao kama mateka. Lakini, ingawaje Mungu aliwaahidi kwamba atawarudisha kwao kutoka Babeli baada ya miaka 70. Mungu alinyan'ganya mfalme wa mwisho taji. Alisema hakutakuwa na mfalme mwingine wa Israeli mpaka atakapokuja mfalme wa haki atawale. Mfalme huyu atakuwa Yesu Kristo atakapokuja kutawala kwa Ufalme wa Mungu hapa duniani.

Watu wa Israeli walioitwa Wayahudi, baadaye walitoka matekani na kurudi kwa nchi ya Israeli tena. Lakini hawakukuwa na mfalme wao. Walitawaliwa na wafalme wa mataifa mengine.

Mungu alituma Mwanawe Yesu Kristo awe Mwokozi tena Mfalme wa Wayahudi. Lakini Wayahudi wengi walikataa Yesu. Yesu alifundisha watu juu ya Ufalme wa Mungu. Aliwambia mifano mingi kuhusu Ufalme wa Mungu ujao. Lakini wengi wao hasa watawala, hawakumwamini.

Yesu alijua watawala watamuua, kwa hivyo aliwambia kitakacho fanyika kwa sababu walimkataa. Yesu alitabiri kwamba Yerusalemu itaharibiwa kwa ajili ya uovu wa Wayahudi. Yesu alilia mji na akasema kwamba utazungukwa, watu watauawa na Yerusalemu itaharibiwa kabisa.


Viongozi wa Wayahudi walishauriana kuangamiza Yesu. Walimshika na kusema uongo juu yake kwa Pilato. Wayahudi walipaza sauti wakisema, “Msulibishe! Msulibishe! Damu yake iwe kwetu na watoto wetu.” Kwa hivyo Yesu alisulibishwa.

Kuuwawa kwa Mwana wa Mungu kulikuwa kubaya sana kufanywa na watu wake. Yesu alikuwa ametabiri kwamba Yerusalemu itaharibiwa. Wakati huo Israeli ilitawaliwa na Warumi. Mwaka wa 70 baada ya Yesu, jeshi la nguvu la Warumi lilizingira Yerusalemu. Waliichukua na kuiharibu kabisa pamoja na Hekalu. Baadhi ya watu wengi waliuawa. Wayahudi walitolewa kwa nchi yao na kutawanyishwa kwa mataifa mengine dunia mzima.

Wayahudi wote walifurushwa kutoka kwa nchi yao. Wengi waliuzwa kama watumwa. Wayahudi walitawanyika katika mataifa mengine ulimwengu mzima. Wayahudi wamebaki hivyo kwa karibu miaka 2,000. Wameumia na kudhulumiwa kwa hayo mataifa walikoenda. 🕮 **Soma** Kumbukumbu 28:64 – 67. Hizi mistari zinatuelezea mateso yatakayo wapata Wayahudi kwa sababu ya kukataa kutii Mungu. Watatawanyishwa kwa mataifa yote ya ulimwengu. Hawatapumzika. Wataishi wakihofia maisha yao usiku na mchana. Haya ni kweli yalifanyika kwa Wayahudi.

Mungu aliadhibu hawa watu kwa sababu ya uovu wao. Lakini hakuwasahau. Hakuwaadhibu milele. Kabla ya kutawanyika, Mungu aliwaahidi kwamba siku moja watarudi kwa nchi yao.

Mungu amewatenga Wayahudi kutoka kwa watu wengine popote walikoenda kwa karibu miaka 2,000. Kwa karne hii, Mungu amekuwa akitengeneza mambo ili awarudishe watu wake kwa nchi yao vile alikuwa ameahidi. Wakati wa vita vya dunia vya 2, Wajeremani walitesa Wayahudi. Zaidi ya Wayahudi milioni 6 waliuwawa na Hitla. Mwisho wa vita, ulimwengu mzima ulikuwa na hofu kwa ajili ya yale yaliyotendeka kwa Wayahudi kwa hivyo waliwarudishia nchi yao.



*Bendera ya Israeli*

Tarehe 14-05-1948, taifa la Israeli lilisimamishwa na Wayahudi wote ulimwenguni walifurahi. Tangu wakati ule, Wayahudi wamerudi Israeli kutoka nchi zingine. Wayahudi sasa wana bendera yao na pesa zao. Lugha ya kitaifa ni Kiebrania.

Wayahudi wamefanya bidii sana kwa nchi yao yenye ilisahuliwa na kuwa kame. Sasa inarotuba, na inakilimo kizuri na inazalisha sana. Israeli imekua sana kifedha na uchumi kutoka kwa viwanda.

Kila siku Wayahudi wako wanarudi kwa nchi ya Israeli. Kila siku Mungu anaendelea kufanya kusudi ya kuwarudisha Wayahudi kwa nchi yao vile aliwaahidi. Kwa sasa kuna Wayahudi zaidi ya milioni 6 kwa nchi ya Israeli.

Watu wa Mungu sasa wamerudi kwa nchi yao baada ya miaka 2,000. Kusimama kwa taifa la Israeli na kurudi kwa Wayahudi, ni ishara kuu kwamba Yesu ako karibu kuja. Tunaona Mungu anaendelea kufanya kusudi lake kwa kuwarejeza watu wake.

Leo hii Wayahudi wengi hawaamini kwamba Yesu ni Mwana wa Mungu. Hawaamini kwamba Mungu ndiye aliwarudisha kwa nchi yao. Wanafikiri wamefanya hivyo kwa nguvu zao.

Wayahudi wamezingirwa na maadui. Mataifa ya Waarabu hawawapendi na huwa wanataka kuwaangamiza. Mwishowe mataifa mengi watakuja kuwapiga Wayahudi. Lakini Yesu atakuja na kuwaokoa  Wayahudi watu wake. Yesu atawaonyesha Wayahudi mashimo ya misumari yenye walimpigilia wakimsulibisha. Atawaonyesha mahali penye walimchoma mkuki kwa ubavu. Hapo sasa Wayahudi wataamini. Watalia kwa sababu walimkataa Yesu na hawakumwamini.

Yesu ataanza kutawala Wayahudi kwa nchi ya Israeli. Wayahudi wenye bado wanaishi kwa mataifa mengine watarudi kwa nchi yao ya Israeli. Wayahudi na nchi ya Israeli itakuwa katikati ya Ufalme wa Mungu hapa duniani. Yesu atatawala kutoka Yerusalemu kama mji mkuu.

Hii itatimiza ahadi ya Mungu kwa Ibrahimu. Ibrahimu atafufuliwa kutoka kwa wafu. Ataishi milele kwa nchi ya Israeli aliyoahidiwa na Mungu. Hata Daudi naye atafufuliwa kutoka kwa wafu. Ataona ahadi za Mungu kwake zikitimizwa kwa kuona Yesu akitawala kwa kiti kilichokuwa chake Yerusalemu. Daudi atakuwa mkuu akisaidia Yesu kutawala Wayahudi kutoka Yerusalemu. Yesu aliahidi wanafunzi wake 12 kwamba watakaa kwa viti vya enzi wakitawala kabila 12 za Israeli. Nao watafufuliwa kutoka kwa wafu na watawale kabila za Israeli kwa Ufalme wa Mungu.